

Kuhamishia miche kwenye kitalu kikubwa

Baada ya miezi 3 ya kitalu cha awali, miche inakuwa tayari kuhamishiwa kwenye kitalu kikubwa. Hatua za uanzishaji wa kitalu kikubwa hazina tofauti na zile za kitalu cha awali isipokuwa;-

1. Saizi ya kiriba katika kitalu kikubwa ni inchi 14 upana kwa inchi 18 urefu.
2. Viriba hupangwa kwa nafasi ya mita 0.8 mstari kwa mstari na mita 0.8 shina kwa shina.



Namna ya kupanda

1. Jaza udongo uliochanganywa na samadi na mchanga kwenye viriba vikubwa ujazo wa nusu ya kiriba.
2. Chukua kiriba kidogo chenye mche, chana karatasi ya kiriba na kuiondoa.
3. Weka mche kwenye kiriba kikubwa, hakikisha mche unakaa katikati ukiwa na udongo wake.
4. Jazia udongo kwa kuuzungushia mche ulioupandikiza hadi juu kisha shindilia



Utunzaji wa kitalu

1. Viriba vimwagiliwe maji kwa kuhakikisha udongo una unyevu wa wastani kila wakati.
2. Maji yamwagiliwe wakati wa asubuhi au jioni na isiwe mchana.
3. Palilia kitalu chako kwa kuondoa magugu na hakikisha kinakuwa safi kila wakati.
4. Tumia mbolea ya NPK (gramu 5 kwa kiriba) kama utaona miche yako inakuwa na unjano kwenye majani
5. Dhibiti magonjwa, fangasi na wadudu



Faida za kitalu

1. Ni rahisi kuhudumia kutokana na udogo wa eneo la kitalu.
2. Hupunguza gharama za kutunza miche tofauti na kama ingehudumiwa ikiwa shambani.
3. Ni rahisi kudhibiti magonjwa pamoja na wadudu waharibifu.
4. Hutoa fursa ya kuchagua miche bora ya kupeleka shambani kwa kuitoa miche iliyo dhaifu.
5. Huruhusu miche ikomae na istahimili mazingira ya shambani kama ukame,



UANZISHAJI NA UTUNZAJI WA KITALU CHA MICHE YA MICHIKICHI



Kimetayarishwa na;

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)
Kituo cha Kihinga
S.L.P 132,
KIGOMA
Email: cdkihinga@tari.go.tz

Utangulizi

Kitalu ni eneo linalotumika kukuzia miche baada ya kuoteshwa na kabla ya kupandwa shambani. Ukuzaji wa miche ya michikichi kwenye kitalu umegawanyika katika hatua kuu mbili. Hatua ya kwanza ni **kitalu cha awali** (primary nursery) ambapo miche hukaa kwa muda wa miezi mitatu tangu kuota na hatua ya pili ni **kitalu kikubwa** (main nursery) ambapo miche hukaa miezi 6 hadi 9 baada ya kutoka kwenye kitalu cha



Uchaguzi wa eneo la kitalu

1. Eneo liwe karibu na chanzo cha uhakika cha maji.
2. Eneo liweze kufikika vizuri ili kurahisisha shughuli za usafirishaji wa miche.
3. Eneo lisiwe na mteremko mkali ili kurahisisha shughuli za utunzaji kitalu.
4. Eneo lisiwe mbali na udongo

Mahitaji ya msingi ya kitalu cha awali

1. *Zana*: Jembe, ndoo, keni za kumwagilia, sepetu, kamba na chekecheo la udongo.
2. *Pembejeo*: Mbolea na viriba.
3. *Udongo wa msituni*: Udongo uwe na rutuba ya kutosha.
4. *Udongo wa kichanga*:
5. *Samadi*: Samadi iliooza vizuri.

Hatua za uandaaji wa kitalu cha awali

A. Kuandaa mchanganyo wa udongo

1. Chekecha udongo wa msituni na mchanga ili kuondoa mawe, takataka na magugu kwenye udongo.
2. Changanya udongo wa msituni, samadi na mchanga kwa uwiano wa 3:2:1 (udongo 3: samadi 2: mchanga 1) kwa kutumia chepe huku ukiongeza maji kidogo kidogo kuufanya udongo uwe na unyevu unyevu bila kutengeneza tope.

B. Ujazaji wa udongo kwenye viriba

1. Jaza mchanganyiko wa udongo kwenye viriba (inchi 5 upana na urefu inchi 7) kwa kujaza nusu ya kitako cha kiriba. Shindilia iwe ngumu ili udongo usimwagike.
2. Kamilisha kujaza sehemu iliyobakia na uhakikishe viriba havina mikunjo baada ya kujaza achia sm 1 kutoka juu ya kiriba.
3. Panga viriba vilivyojazwa kwenye sehemu safi iliyoandaliwa kwa ajili ya kitalu kwa

C. Upandaji wa mbegu kwenye viriba

1. Mwangilia maji kwenye viriba kabla ya kupanda kama viriba vyako vitakuwa vimekauka.
2. Fukua shimo dogo katikati ya kiriba kisha weka mche uliyoota kwa kutanguliza sehemu ya mzizi chini



na ya shina juu.

3. Funika mche kwa udongo kiasi cha sentimeta 2 kutoka juu ya usawa wa kiriba.
4. Weka kivuli kwenye kitalu kwa kujengea vichanja vya nyasi kama

